

## GRADE 5 MID TERM 3 DECEMBER 2021

### KISWAHILI

#### **SEHEMU YA KWANZA**

##### **I. Kusikiliza na kuzungumza (Alama 5)**

**Mwalimu atauliza mwanafunzi maswali yafuatayo naye mwanafunzi ayajibu.**

- a) Salamu kwa heri hujibiwaje? (alama 1)  
**(Mwanafunzi ajibu)**
- b) Eleza jinsi utamsaidia rafiki yako akiumia uwanjani mnapocheza  
**(Mwanafunzi ajibu)** (alama 1)
- c) Eleza kile utafanya ili kuzuia ajali au kuumia wakati mnacheza  
**(Mwanafunzi ajibu)** (alama 1)
- d) Mtu akipata ajali anafaa kupelekwa wapi? (alama 1)  
**(Mwanafunzi ajibu)**
- e) Mtu anayewahudumia wagonjwa hospitalini huitwaje? (alama 1)  
**(Mwanafunzi ajibu)**

## **II. KUSOMA KWA SAUTI**

**Soma kifungu kifuatacho kwa sauti mwalimu akisikiliza.**

Ajali za barabarani zinazidi kuwa nyingi humu nchini. Ajali hizi za barabarani zinasababisha vifo vya watu wengi sana.

Ajali za barabara husababishwa na mambo chungu nzima. Kwanza kuna wale madereva ambao hawafuati sheria za barabarani. Pia kuna wale madereva wanaoendesha magari wakiwa walevi. Isitoshe, kuna yale magari yaliyo katika hali mbovu. Haya magari hayastahili kuwa katika barabara zetu.

Wale wanaotembea kando ya barabara pia husababisha ajali wakikosa kuzingatia sheria za barabara.


Waendeshaji pikipiki pia hawawezi kuachwa nyuma. Wao husababisha ajali nyingi sana barabarani. Pia kuna barabara ambazo ni mbovu zilizo na mashimo.

Kila mtu anastahili kuwa mwangalifu anapotumia barabara. Hii itasaidia kuepuka ajali barabarani na kuzuia vifo vya watu kutokana na ajali.


## **IV. SARUFI (Alama 20).**

### **1. Andika majina ya vifaa hivi. (alama 5)**


a)




b)




c)



(d)



(e)



**2. Andika sentensi kwa kutumia vitenzi vifuatavyo. (alama 5)**

- a) Vaa \_\_\_\_\_
- b) Faa \_\_\_\_\_
- c) Fua \_\_\_\_\_
- d) Vuta \_\_\_\_\_
- e) Futa \_\_\_\_\_

**3. Pigia mstari nomino ya kawaida katika sentensi. (alama 5)**

- a) Atieno ameingia katika darasa.
- b) Mwalimu atarudi tena.
- c) Walienda Nairobi kwa kutumia basi.
- d) Leo ni siku yangu ya kuzaliwa.
- e) Ninahitaji kalamu yangu.

**4. Andika wingi wa nomino zifuatazo (alama 5)**

- a) Uji \_\_\_\_\_
- b) Maji \_\_\_\_\_
- c) Sukari \_\_\_\_\_
- d) Ugali \_\_\_\_\_
- e) Chumvi \_\_\_\_\_

### **III. UFAHAMU (Alama 5).**

#### **Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali.**

Teknolojia inatusaidia kufanya mambo mengi sana. Ukitaka kujua yanayofanyika humu nchini na hata duniani kote, utatumia teknolojia. Ukitaka kurekodi na kutazama video kuhusu somo au jambo fulani utahitaji teknolojia. Pia ukitaka kupiga picha au kutazama picha ya kitu fulani, utahitaji teknolojia.

Kuna aina nyingi ya vifaa vya teknolojia. Kwa mfano, tarakilishi ambayo pia huitwa kompyuta na rununu ambayo pi huitwa simu ya mkono.

Runinga na kikokotozi pia ni vifaa vya teknolojia. Kikokotozi hutumiwa kupigia hesabu. Runinga nayo hutusaidia kutazama vipindi maalum. Pia sisi hupata habari kuhusu matokeo fulani kupitia runinga.

- a) Andika faida mbili za teknolojia **(alama 2)**

---

---

- b) Taja vifaa vitatu vya teknolojia **(alama 3)**

---

---

---

- c) Ni kifaa gani hutusaidia kupiga hesabu? \_\_\_\_\_ **(alama 1)**

- d) Tazama kifaa hiki kisha uandike jina lake \_\_\_\_\_ **(alama 1)**



- e) Jina jingine la kompyuta ni gani? \_\_\_\_\_ **(alama 1)**

- f) Andika faida mbili za runinga? **(alama 2)**

---

---